**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# CHUO CHA UALIMU MANDAKA

Anuani ya Simu: 0738564848
E-mail: mandakatc@gmail.com
mandakatc@moe.go.tz
website: www.mandakatc.ac.tz
Simu: +255738564848

MTAA WA MRERENI
KATA YA KILEMA KUSINI
S.L.P 725,
**MOSHI**
**KILIMANJARO**

**Kumb.Na.MTC/STJ/21/VOL.VI/02**

Tarehe: **30/05/2025**

JINA:-……………………………………….
……………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026**

1. **UTANGULIZI.**

Uongozi na Jumuiya yote ya Chuo cha Ualimu Mandaka wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi mchepuo wa Sayansi na Hisabati (kwa kutumia lugha ya kiingereza). Hongera sana! Ni tunu kupata nafasi ya kuchaguliwa kusomea Taaluma ya ualimu ambayo ni taaluma mama ya taaluma nyingine zote. Itumie vema nafasi hiyo ili katika kipindi chako cha mafunzo uweze kujijengea maarifa, stadi na mwelekeo wa kutosha kukidhi mahitaji ya Mwalimu bora katika viwango vya sasa na baadaye katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

Mafunzo ya Ualimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi (Miaka miwili) yameandaliwa kwa lengo la kuwajengea umahiri wa kitaaluma na kitaalamu walimu watakaofundisha katika shule za msingi ili kumudu ufundishaji, malezi ya wanafunzi, utafiti wa Kielimu na uendeshaji wa shule kwa ufanisi.

Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu Msingi ni ya miaka miwili **(2)**. Unatakiwa kuripoti chuoni kuanzia **tarehe 18/08/2025** na mwisho wa usajili ni **tarehe 30/08/2025.** Unatakiwa kufika chuoni ndani ya tarehe hizo zilizotajwa bila kukosa.

Aidha, napenda kukufahamisha kuwa kusoma Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi katika masomo ya Sayansi na Hisabati kunakuwezesha kupata mkopo wa Elimu ya Juu kama utahitaji. Hivyo, hii ni fursa ya kipekee kabisa kwa wanachuo wa masomo hayo, unaweza kutembelea bodi ya mkopo kupitia tovuti https://olas.heslb.go.tz ili kupata maelezo Zaidi.

**MAHALI CHUO KILIPO NA USAFIRI WA KUKUFIKISHA CHUONI.**

(a) **Mahali Chuo kilipo**
Chuo cha Ualimu Mandaka kipo Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Moshi vijijini, kata ya Kilema Kusini karibu na mji wa Himo.

(b) **Jinsi ya kufika Chuoni**

- Ukiwa unatokea Moshi mjini elekea kituo kikuu cha mabasi, panda mabasi (hiace) yanayoenda Himo/Holili/Mwika/Marangu/Kilema na uteremke kituo cha Himo Mjini.
- Ukitokea njia kuu ya Tanga/DSM teremka stendi ya mabasi ya Njiapanda na panda gari zinazoelekea Himo Mjini.
- Kutoka Himo Mjini, panda magari yanayoelekea **Kilema** kwa **Lazari** na teremka kituo cha **Mandaka. Inakadiriwa kuwa umbali kutoka himo mpaka chuoni Mandaka ni kama kilomita saba (7).**

**Dira, Dhima na Motto wa Chuo**

- **Dira ya Chuo**: Kuwa Chuo Bora cha Ualimu Nchini Kinachoandaa Walimu Mahiri kwa Maendeleo Endelevu
- **Dhima ya Chuo**: Kuhakikisha kuna mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuboresha miundombinu na mifumo inayowezesha kutoa elimu bora na fursa sawa kwa wote.
- **Moto wa Chuo:** Taaluma, Usafi na Uzalishaji Mali.

2. **MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI**

(a) **Vyeti na hati za utambulisha**

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa uje na **vyeti halisi** na **halali** vifuatavyo:-

i. Vyeti vya Taaluma **(Academic Certificates)** vya Kidato cha sita (**VI)** kama unacho au hati ya matokeo **(Result Slip)** kwa wanaotumia sifa za kidato cha sita.
ii. Cheti cha kidato cha nne (CSEE) kwa wote.
iii. Cheti cha Astashahada ya Ualimu kwa wanaotumia sifa za Astashahada.
iv. Cheti cha Kuzaliwa **(Birth Certificate)**
v. Kitambulisho au namba ya **NIDA**
vi. Kadi ya Bima ya Afya kama unayo.
vii. Hati yoyote ya ziada inayoweza kusaidia kukutambulisha na kuthibitisha uhalali wako na uhalali wa umiliki wa nyaraka zako za Kitaaluma na Kitaalamu. Kama huna vyeti halisi **hutapokelewa.**

Kila mwombaji wa Mafunzo ya Ualimu aliyechaguliwa ili asajiliwe anapaswa kulipa Ada na michango kama ifuatayo:-

(b) **Ada.**

Ada ya Mafunzo kwa mwaka ni Tsh.**450,000/=** unaweza kulipa yote au ukalipa Tsh.**225,000/=** kwa muhula. Kabla ya kwenda Benki kulipa wasiliana na Mhasibu wa Chuo simu namba **0755050306/ 0715050306** kwa ajili ya kupewa Control Number (Namba ya uthibiti wa malipo). **Kisha nenda benki yoyote au wakala au lipa kwenye mitandao ya simu kama M-pesa, Mixx by Yas, Airtel- money, n.k.**

(c) **Michango.**

| S/N | MICHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1 | Huduma ya kwanza | Tsh.10,000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Usafi na mazingira | Tsh.20,000/= | Kwa mwaka |
| 3 | Kukodisha godoro | Tsh.10,000/= | Kwa mwaka |
| 4 | Michezo | Tsh.30,000/= | Kwa mwaka |
| 5 | Usajili na Kitambulisho | Tsh.20,000/= | Kwa mwaka wa kwanza tu |
| 6 | Bima ya Afya | Tsh.50,400/= | Kwa mwaka kwa mwanachuo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ambaye hana bima ya afya |
| 7 | Ulinzi | Tsh.30,000/= | Kwa mwaka |
| 8 | Ukarabati | Tsh.25,000/= | Kwa mwaka |
| 9 | Serikali ya wanachuo | Tsh.5,000/= | Kwa mwaka |
| | **JUMLA** | **Tsh.200,400/=** | |

Michango yote namba **1-9** hapo juu ilipwe Benki ya **NMB** Akaunti Namba:- **40301000055** Jina la Akaunti **Principal Mandaka T.C.**
**NB:** Kwa malipo yote ya **Michango** utakayolipa Benki, ***Tumia jina rasmi la mwanachuo kama lilivyoandikwa kwenye vyeti vyake vya kufuzu Elimu ya Sekondari***. Hakikisha una hati halisi **(Bank Pay In Slip)** ya kulipia fedha hizo. Tafadhali zingatia tofauti ya namna ya kulipa Ada na michango kama zilivyotajwa hapo juu. **HATUPOKEI FEDHA TASLIMU.** Hata kama umeomba mkopo, utapaswa kulipa ada na michango. Kama utapata mkopo utarejeshewa fedha uliyolipa.

(d) **Sare ya Chuo.**

1. **Sare ya Chuo wasichana.** Jozi mbili shati la mikono mirefu rangi ya bluu bahari **(light blue)** suti nyeusi, sketi ndefu yenye V mbele na koti la mikono mirefu tai ndefu ya bluu yenye mistari meupe. **Unaweza kuipata hapa chuoni au ukashona mwenyewe, isiwe ya mtumba**. Kwa wasichana wa Kiislamu hijabu iwe kitambaa cheusi kisiwe na urembo aina yeyote. **Nunua kabla ya kuripoti Chuoni.**

2. **Sare ya Chuo wavulana**. Jozi mbili shati la blue bahari **(light blue)** la mikono mirefu, suti nyeusi - suruali na koti la mikono mirefu, tai ndefu ya bluu yenye mistari myeupe, Suruali iwe na luksi kwa ajili ya kufungia mkanda upana wa chini isipungue inch 16, iwe na mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma wenye kifungo**. Suruali isiwe ya kubana (Modo).** Sare ya Chuo unaweza ukashona katika maeneo ya karibu na Chuo baada ya kufika Chuoni. **Sare ya Chuo isiwe ya mtumba**

3. **Sare ya viatu kwa wote**.
Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika miguu visiwe na visigino virefu jozi mbili soksi nyeusi kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
**N.B** utatakiwa kuvaa sare ya Chuo na mavazi **NADHIFU** na ya **HESHIMA** yanayoendana na Maadili ya Ualimu wakati wote.

4. **Mavazi ya michezo.**
Traki-suti, yenye nembo ya Chuo rangi nyeusi inapatikana chuoni kwa bei ya **Tsh.25,000/=**. Mwanachuo atahitajika kuja na T-shirt rangi ya blue, bukta rangi ya blue na raba za michezo. Pia, kuna siku za kuvaa T-shirt, hivyo unatakiwa kuwa na T-shirt yenye Nembo ya Chuo - Tsh.**15,000/= (itapatikana chuoni).**

5. **Mahitaji kwa ajili ya malazi.**
Bed cover nyeupe, pazia zito rangi nyeupe kwa ajili ya dirisha la chumba utakachokuwa unalala (ft 4x6), chandarua ya kuzuia mbu ft 3x6, uje na mto na foronya nyeupe, blanket moja zito, Shuka mbili rangi ya 'light blue' - bluu bahari [wavulana], shuka mbili rangi ya pink (wasichana), ndoo na vifaa vya chakula. **NB:-**

**(vifaa hivi vinapatikana duka la chuo). Vyombo vya chakula visiwe vya plastiki.**

6. **Mahitaji ya lazima kwa ajili ya Taaluma.**
   - Utahitajika kununua na kuja na Mihtasari ya masomo ya shule ya msingi. Chagua vitabu vinavyohusiana na masomo aliyochaguliwa kusomea
   - Counter book **10 angalau Q2**
   - Mafaili ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za kitaaluma kulingana na tahasusi unayosomea (Stashahada Ualimu Elimu ya Msingi 10)
   - Bunda moja la karatasi (ream – nopa) zinapatikana duka la Chuo
   - Vitabu na machapisho mengineyo kulingana na tahasusi unayosomea

7. **Afya.**
   (a) Ili uweze kukubaliwa kusomea Mafunzo ya Ualimu unahitajika kupimwa afya yako na kuthibitishwa na Daktari wa Serikali kwa kujaza fomu (Request for Medical Examination) iliyoambatanishwa ambayo utakuja nayo Chuoni.
   Hakikisha kuwa fomu hiyo imepigwa muhuri wa Ofisi ya Daktari mhusika.
   Aidha, unaweza kuhitajika na Mkuu wa Chuo kupimwa afya yako wakati wowote unapokuwa Chuoni.
   (b) Mwanachuo mwenye uja uzito hatapokelewa Chuoni
   (c) Kwa kupitia mchango wa huduma ya kwanza utakaotoa unapojiunga, na baadaye kila mwaka, Chuo kitatoa Huduma ya Kwanza katika Zahanati ya Chuo. Matibabu mengine nje ya zahanati ya Chuo utatumia Bima ya afya.
   (d) Chuo kinatoa huduma ya chakula lakini hakitatoa huduma ya chakula maalum **(Light or Special diet)** kwa wanachuo wenye matatizo ya kiafya.

8. **Mahitaji Mengine.**
   Mahitaji mengine madogo madogo kama vifaa vya usafi binafsi, vyombo vya chakula, matumizi ya photocopy na zana za Kujifunzia na Kufundishia utajinunulia mwenyewe ufikapo Chuoni baada ya kupewa maelekezo. Hakikisha una fedha za matumizi binafsi.

9. **Kanuni na Taratibu.**
   - Ufikapo Chuoni utapaswa kufuata Kanuni na Taratibu zinazoongoza mwenendo na mahitaji ya Mafunzo ya Ualimu. Miongozo hiyo ya Kanuni, Taratibu na Sheria za Chuo imewekwa ili kuhakikisha kuwa viwango vya utendaji Kitaaluma na mwenendo wa mwanachuo kwa ujumla vinakidhi vigezo vya Mafunzo ya Ualimu.
   - Kwa ujumla wake taratibu na Kanuni za Mafunzo ya Ualimu haziruhusu unywaji wa pombe, ulevi wa aina yoyote ile na tabia zote zisizo za Kimaadili. Baada ya Kusoma Kanuni na Sheria za Chuo utajaza fomu ya kukubali Kujiunga na Mafunzo kabla ya kusajiliwa. Kujisajili maana yake ni kuridhia kuzifuata Kanuni na Sheria za Chuo wakati wote utakapokuwa Chuoni.

10. Endapo utakwama na unahitaji msaada au ufafanuzi zaidi wasiliana na watendaji Wafuatao:- **L. Kiria – Msajili wa Chuo – Simu 0766 935313**

**NB: ZINGATIA MUDA WA KUPIGA SIMU NI SAA ZA KAZI TU (1:30-9:30 ALASIRI) VINGINEVYO IWE NI DHARURA.**

**Taarifa zote muhimu,** zinazomhusu mwanachuo anapokuwa chuoni, mfano maafa, msiba, ugonjwa, n.k. toka nyumbani **lazima zipitie** kwa **Mkuu wa Chuo** na **siyo** kwa mwanachuo.

**Mwisho.**
Kumbuka kuwa siku zote Mwalimu anapaswa kuwa mfano bora wa kuigwa kwa matendo mazuri kwa wanafunzi wake na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo kila mwanachuo anatazamiwa awe na tabia nzuri na mwenendo unaoakisi maadili ya ki-ualimu wakati wote wa Mafunzo yake na baada ya Mafunzo yake.

Jumuiya ya Chuo cha Ualimu Mandaka inakupongeza na kukukaribisha Kujiunga na Mafunzo ya Ualimu.

**UWE NA MAANDALIZI MEMA YA KURIPOTI CHUONI KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU.**
**KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MANDAKA.**

**Isaya. M. Msanga**
**<u>MKUU WA CHUO</u>**
Simu: **0713 781 135 au 0752 442 019**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MANDAKA
HIMO—MOSHI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# CHUO CHA UALIMU MANDAKA

Anuani ya Simu: 0738564848
E-mail: mandakatc@gmail.com
mandakatc@moe.go.tz
website: www.mandakatc.ac.tz
Simu: +255738564848

MTAA WA MRERENI
KATA YA KILEMA KUSINI
S.L.P 725,
**MOSHI**
**KILIMANJARO**

---

**FOMU YA KUKUBALI KUWA MWANACHUO**

ANWANI YAKO:-……………………………
……………………………………..
………………………………………

MKUU WA CHUO,
CHUO CHA UALIMU MANDAKA,
S.L.P. 725,
**MOSHI.**

Mimi…………………………………………………………………………………...............
(Majina rasmi kwa herufi kubwa kama yanavyoonekana kwenye vyeti) nimesoma na kuelewa vizuri maagizo na masharti ya kujiunga na Chuo kwa Mafunzo ya Ualimu kwa mwaka…………………………… hadi ……………………………………..

Ninaahidi kuwa nitayatimiza yote yaliyoandikwa pamoja na kanuni na taratibu nyingine nitakazopewa nifikapo chuoni.

Ninaomba nipokelewe chuoni, na iwapo nitakwenda kinyume cha masharti, kanuni na taratibu hizo, nitakuwa tayari kupokea adhabu nitakazopewa kulingana na makosa nitakayokuwa nimeyatenda.

**SAINI YANGU………………………………………………………………………………**
**TAREHE…………………………………………………………………………………….**

**ZINGATIA: SEHEMU YA CHINI IJAZWE NA MZAZI/MLEZI/MFADHILI TU**
Mimi Mzazi/Mlezi/Mwajiri……………………………………………………………………..…
Nimesoma kwa makini maelezo na kanuni, sheria na taratibu zote za Chuo.
Nipo/sipo tayari kushirikiana na Chuo wakati wote wa mafunzo kuhusu malezi ya kijana wangu.

**SAINI YAKE………………………………….. TAREHE……………………………………..**
**ANWANI YAKE……………………SIMU……………………………E-MAIL………………..….**

Wakati wa likizo, mwanachuo………………………………………………………………...
(Jina la Mwanachuo) atasafiri kurudi kwa Mzazi/Mlezi/Mfadhili wake ambaye yuko;
1. KIJIJI/MJI…………………………………….S.L.P. ………………………………………..
2. KATA YA…………………………………………………………………………………….
3. WILAYA YA……………………………………………………………………………….……
4. MKOA WA……………………SIMU…………………….……………..E-MAIL………………….

**SAINI YA MZAZI/MLEZI/MFADHILI…………………………………………………………….**

(i) Ikumbukwe kwamba wakati wa likizo wanachuo wanasafiri kurudi kwa wazazi au walezi na si Vinginevyo
(ii) Kama kuna sababu yoyote itakayokuzuia kujiunga na chuo hiki, tunaomba usijaze fomu hii isipokuwa jina lako tu, uitume fomu hii kwetu. Ni kitendo cha kiungwana kutoa taarifa.

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: The Medical Officer,

……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

From: **The Principal,**
Mandaka Teachers' College,
P. O. Box 725,
**Moshi.**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MANDAKA
HIMO—MOSHI

**Mr/Miss/Mrs**…………………………………………………………………… (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training course. The examination should include the following categories (I – IV) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

Pregnancy (Category IV) will also render a girl ineligible for the course.

i) (a) Eye-sight (e) Leprosy
(b) Hearing (f) Limbs
(c) Speech (g) Epilepsy
(d) Venereal Diseases

ii) Neuroses (iii) Other serious diseases (iv) Pregnancy

---

**PART B:** **<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**

(To be completed by a Government Medical Officer)
I have examined the above named and considered that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full-time teacher training course.

a) Eye-sight ……………………………………………………………………………
b) Hearing ……………………………………………………………………………..
c) Limbs ……………………………………………………………………………….
d) Venereal diseases……………………………………………………………..…
e) Leprosy ……………………………………………………………..……..………
f) Epilepsy…………………………………………………………..………………..
g) Neuroses …………………………………………………………..…………..………
h) Other serious diseases ………………………………………………………………
i) Pregnancy ……………………………………………………….……………………

Date ………………………………… Signature ………………………………..…………..

Station ……………………………… Designation ……………………… Mhuri………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# CHUO CHA UALIMU MANDAKA


Anuani ya Simu: 0738564848
E-mail: mandakatc@gmail.com
mandakatc@moe.go.tz
website: www.mandakatc.ac.tz
Simu: +255738564848

MTAA WA MRERENI
KATA YA KILEMA KUSINI
S.L.P 725,
**MOSHI**
**KILIMANJARO**


---

## FOMU YA KUMBUKUMBU ZA MWANACHUO

Bandika picha hapa

1. JINA KAMILI………………………………………………………………………
2. MWANAUME/MWANAMKE……………………………………………………
3. NIMEOA/SIJAOA/NIMEOLEWA/SIJAOLEWA/Fr/Sr. ………………………..
4. TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………...
5. URAIA……………………………………….KABILA…………………………
   DINI (DHEHEBU)……………………………………………………………….
6. ANUANI YA NYUMBANI…………………………………………………….
   …………………………………………………………………………………………..
7. JINA LA BABA/ MLEZI……………………………………………………………...
8. ANUANI YAKE ……………………………………………………………………..
   ……………………………………………………………………………………………..
9. KAZI YA BABA/ MLEZI ……………………………………………………………
10. NAMBA YAKE YA SIMU……………………………………………………………
11. JINA LA MTU WA KARIBU NA MZAZI…………………………………………………
12. NAMBA YAKE YA SIMU……………………………………………………………
13. ANUANI YAKE………………………………………………………………………….
    ……………………………………………………………………………………………..
14. ELIMU YA MSINGI DARASA LA I-VII: MWAKA………………….HADI……………..
15. ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA I-IV MWAKA…………… HADI……………..
    SHULE YA SEKONDARI ULIYOSOMA……………………………………………
16. MASOMO YA KIDATO CHA NNE NA UFAULU ULIOPATA
    1…………………………………( ….)  6……………………………………(….)
    2…………………………………(…..)  7……………………………………(….)
    3…………………………………(…..)  8……………………………………(….)
    4…………………………………(…..)  9……………………………………(….)
    5…………………………………(…..)  10…………………………………..(….)
17. INDEX NAMBA YA CHETI CHA KIDATO CHA IV ……………………………..…
18. ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA V-VI AU GATCE MWAKA…………… HADI……………..
    SHULE/CHUO……………………………………………………………...
19. MASOMO YA KIDATO CHA VI/GATCE NA UFAULU ULIOPATA:
    1………………………………..(….)  6……………………………………(….)
    2………………………………..(….)  7……………………………………(….)
    3………………………………..(….)  8……………………………………(….)
    4…………………………………(….)  9……………………………………(….)
    5…………………………………(….)  10…………………………………(….)

20. INDEX NAMBA YA KIDATO CHA VI/GATCE ……………………………………………………..
21. KAZI ULIZOWAHI KUFANYA BAADA YA KUMALIZA SHULE:
    ……………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..
22. MWAJIRIWA / SIO MWAJIRIWA ……………………………………………..
T.S.C. NO. ………………………………… CHECK NO. …………………………………..
23. TAREHE YA KUANZA KAZI……………………………………………………………..
24. MWAJIRI WAKO………………………………………………………………………..
25. ANUANI YA MWAJIRI ………………………………………………………………………….…
26. NIMEOA/NIMEOLEWA/SIJAOA/SIJAOLEWA…………………………………………………
27. JINA LA MWENZA WAKO………………………………………….. SIMU……………………
28. MAJINA YA WATOTO WAKO (KAMA UNAO) NA UMRI WAO
1. ……………………………………(…..) 3. ……………………………………(…..)
2. ……………………………………(…..) 4. ……………………………………(…..)
29. SHULE ULIZOWAHI KUFUNDISHA:

| **NA** | **SHULE** | **MWAKA** | **HADI** | **MADARAKA** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

30. JINA LA ANAYEGHARAMIA MAFUNZO YAKO ………………………………………………..

31. ANWANI YAKE……………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………..……………
NAMBA ZAKE ZA SIMU ….……………………………………………………………………
32. STADI NYINGINEZO ULIZONAZO MFANO UFUNDI/ MICHEZO/UCHORAJI, N.K.
……………………………….......................................................................................
…………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………..
33. ANDIKA MASOMO YAKO YA STASHAHADA UTAKAYOSOMA.
1. ………………………………………….. 6. …………………………………………
2. ………………………………………….. 7. ………………………………………….
3. ………………………………………….. 8. ………………………………………….
4. ………………………………………….. 9. ………………………………………….
5. ………………………………………….. 10. …………………………………………

NATHIBITISHA KUWA TAARIFA HIZI NILIZOTOA NI KWELI TUPU NA ENDAPO ZITATHIBITIKA KUWA NI ZA UDANGANYIFU SHERIA ICHUKUE MKONDO WAKE.

NAMBA YA SIMU…………………………

………………………… ……………………….
SAINI YAKO TAREHE

34. DINI ………………………….. DHEHEBU …………………………………

35. JINA NA SAINI YA MSAJILI………………………………….. TAREHE…….……………….

****** Kata isiyohusika***